

Maswali

1. Paulo alitumwa atoke kwa mji gani aende ahubiri Injili?
2. Paulo alienda na nani?
3. Walienda kwa kisiwa gani?
4. Nani aliamini Injili huko Kipro?
5. Nani alijaribu kumgeuza Sergio Paulo kinyume na Paulo na Injili?
6. Nini ilifanyika kwa Elima?
7. Paulo alifanya muujiza gani huko Listra?
8. Watu walidhani Paulo na Barnaba ni nani?
9. Mbona Paulo alighadhabika sana kwa sababu watu walitaka kumtolea dhabihu?
10. Nini ilitendeka kwa Paulo Wayahudi walipokuja kutoka Antiokia

Majibu

1. Paulo alitumwa kutoka Antiokia aende ahubiri Injili.
2. Paulo alienda na Barnaba.
3. Walienda kwa kisiwa cha Kipro.
4. Sergio Paulo Liwali wa Kirumi aliamini Injili.
5. Elimu alijaribu kumshawishi kinyume na Paulo na Injili.
6. Paulo alimfanya Elimu akawa kipofu.
7. Paulo aliponya mtu kipofu huko Listra.
8. Walidhania wao ni miungu. Paulo – Herme na Barnaba – Zeu
9. Mungu ni Mungu mmoja aliye wa kweli. Paulo alikuja kubadilisha watu wasiabudu miungu wa uongo.
10. Walipiga Paulo kwa mawe, na kumtupa nje ya mji wakifikiria kwamba amekufa.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



95 Paulo anahubiri Injili

Kwa Biblia


Matendo ya Mitume 13:1 – 12 na 14:8 – 20

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo alisafiri nchi za mbali akihubiri Injili. Mungu alikuwa naye na alimsaidia.

Somo

Kwa somo lilitopita tulijifunza vile Sauli alikuwa Mkristo. Yesu alichagua Sauli kuhubiri Injili kwa Mataifa. Baadaye Sauli alibadilisha jina lake na akawa Paulo. Paulo alienda kuishi kwa mji wa Antiokia. Antiokia ilikuwa na kikundi kikubwa cha Wakristo. Kulikuwa na walimu na manabii wengi.



Antiokia
ya Siria

Siku moja Wakristo walikutana Antiokia pamoja. Roho Mtakatifu aliwambia, "Nimechagua Paulo na Barnaba wahubiri Injili. Waachilie waende waanze kazi."

Wakristo wa Antiokia waliomba baraka kutoka kwa Mungu na wakawaacha Paulo na Barnaba kwenda kuhubiri Injili. Paulo na Barnaba walielekea pwani. Walitumia meli kwenda kwa kisiwa cha Kipro. Kule walikutana na mtu aitwae Sergio Paulo. Alikuwa mtu wa maana. Alikuwa Liwali wa Kipro. Sergio Paulo aliwasikiliza Paulo na Barnaba. Alikuwa na haja sana kusikia injili juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu.


Elima alikuwa mtumishi wa Sergio Paulo. Elima alikuwa nabii wa uongo tena mchawi. Elima alikasirika alipoona Sergio Paulo ana haja na Injili. Elima alikuwa na hofu ya kupotesa kazi yake ikiwa Sergio Paulo atakuwa Mkristo. Mkristo hataamini uchanja wa uchawi wenyewe Elima alikuwa akifanya. Elima alijaribu kushawishi Sergio Paulo aajane na Paulo.

Paulo aliona vibaya sana. Aliambia Elima, "Wewe ni muongo na ni mkora. Hautaacha kujaribu kuficha ukweli wa Mungu? Utakuwa kipofu kwa muda." Papo hapo Elima akaanza kuona kiwi na baadaye giza. Hangeweza kuona. Alizungukazunguka akitaka mtu amwongoze.

Hiki kitendo cha Paulo kilishangaza Sergio Paulo. Paulo alikuwa amefanya huyu mtu muovu kuwa kipofu kwa kutumia nguvu za Mungu. Sergio Paulo aliamini na akabatizwa.

Paulo na Barnaba walikaa na Sergio Paulo kwa muda mchache. Baadaye waliondoka, wakasafiri na kuendelea kuhubiri Injili.

Paulo na Barbaba waliondoka Kipro. Walisafiri kwenda kwa miji zingine za Pisidia ya Antiokia na Ikonia. Walihubiria watu juu ya Yesu na Ufalme wa Mungu. Wayahudi wa hizo miji hawakutaka kuwasikiliza. Walijaribu kupiga Paulo kwa mawe. Paulo na Barnaba waliondolewa hapo.



Paulo na Barnaba walienda Listra. Kulikuwa na mtu kiwete huko Listra. Hakukuwa amewahi kutembea. Huyo kiwete alisikiliza Paulo akihubiri Injili. Na akaamini hiyo Injili. Paulo aliona kwamba huyo kiwete alikuwa na imani. Paulo alimwambia, "Simama kwa miguu yako." Halafu huyo mtu aliruka juu na akatembea.

Watu wa Listra walishangaa. Umati wa watu walikuja kuona huyo mtu akitembea. Watu wa Listra waliamini sana kwa miungu ya uongo. Waliona muujiza wenyewe Paulo alifanya kwa kumfanya mtu kiwete atembee. Walifiiri kwamba lazima Paulo na Barnaba ni miungu yao. Walifikiri Paulo ni mungu Herme na Barnaba ni mungu Zeu.

Kuhani wa Herme mungu wa uongo ametoka hekaluni. Kwa hivyo kuhani walileta fahali na shada za maua. Walitaka watolee Paulo na Barnaba fahali kama dhabihu na wamwabudu kama mungu wao.

Paulo na Barnaba waliudhika sana. Walikuwa wamekuja Listra kufundisha juu ya Mungu mmoja wa kweli. Walikuwa wamekuja kuwambia watu kwamba wasiabudu miungu mingine wala sanamu. Paulo alitoa sauti na kusema, "Msitutolee sisi dhabihu. Sisi ni watu kama nyinyi. Tumekuja kumwambia msiasiabudu miungu mingine wala sanamu. Mungu aliumba kila kitu ulimwenguni. Mungu hutuonyesha sisi nguvu zake na upendo. Hutuletea mvua na jua zitutengenezee chakula tukule." Paulo aliwazuia wasiawatolee dhabihu.

Lakini kulikuwa na Wayahudi walitoka Pisidia ya Antiokia na Ikonia. Waligeuza huo umati kipinga Paulo. Watu walisahahu muujiza wenyewe Paulo alikuwa amefanya. Walisahahu kwamba walikuwa wamefikiria eti Paulo na Barnaba ni miungu. Umati uliokuwa na hasira walipiga Paulo kwa mawe. Wakamburura mpaka nje ya mji wakidhani amekufa.

Lakini Paulo hakukuwa amekufa. Mungu alikuwa ana kazi nyingi sana na Paulo ya kuhubiri Injili. Baada ya muda Paulo alisimama na akarudi Listra. Kesho yake aliondoka akaendelea na safari ya kwenda kuhubiri Injili kwa mji mwingine. Baadaye, Paulo kwa ujasiri, alirudi Listra kuwapa moyo Wakristo walioishi kule.